**HALMASHAURI YA WILAYA YA MUSOMA**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA MENEJIMENTI (CMT) KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUSOMA TAREHE 19/11/2021**

**WATAALAM WALIOHUDHURIA**

1. Ndg. Msongela N. Palela - Mkurugenzi Mtendaji (W)
2. Ndg. Agness Mshiu - Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi
3. Ndg. Victor B. Nyamhanga - Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango
4. Ndg. Tanna Nyabange - Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii
5. Ndg. Ruge G. Kelvin - Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo
6. Ndg. Mbuni Oyundi - Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi
7. Ndg. Jagadi Paschal - Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi
8. Ndg. Kijogi Vicent - Kaimu Mratibu TASAF
9. Adv. Flora Peter - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria
10. Ndg. Mwizarubi E.Nyaindi - Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira
11. Mwl Baraka Maingu - Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
12. Mwl. Sabato Arika - Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
13. CPA. James Kolugendo - Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha
14. TP.. Ester Karatibu - K/Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili
15. Dkt. Athuman Matindo - Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya
16. Ndg. Sophia Manyaki - Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi
17. Ndg. Jaggy Joram - Afisa Usafirishaji

**SEKRETARIETI**

1. Ndg. Mary Mwakalukwa - Mwandishi wa Mikutano
2. Ndg. Emmanuel T. Moke - Mwandishi wa Mikutano

**KUMB. NA. CMT/04/2021/2022/23 KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 04.30 asubuhi na kuwafahamisha wajumbe kwamba ni kikao cha kawaida kwa ajili ya kujadili taarifa ya mapato na matumizi kwa mwezi Oktoba, 2021. Hivyo aliwataka wajumbe kuchangia hoja zilizo mbele yao kwa utulivu kwa maslahi ya Halmashauri, sambamba na kuziboresha taarifa hizo kabla ya kuwasilisha kwenye kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango.

**KUMB.NA. CMT/04/2021/2022/24 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI**

Muhtasari wa kikao cha Timu ya Menejimenti wa tarehe 08/11/2021 uliwasilishwa na kupokelewa, ulisainiwa kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao.

**KUMB.NA. CMT/04/2021/2022/25 YATOKANAYO**

Yatokanayo yaliwasilishwa na kupokelewa, baada ya majadiliano ya kina walimtaka Mweka Hazina (W) atekeleze agizo la wadaiwa walioshinda kesi Mahakamani wanaondolewa kwenye orodha ya wadaiwa.

**KUMB.NA. CMT/04/2021/2022/26 TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KUISHIA MWEZI OKTOBA, 2021**

Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilikisia kukusanya kiasi cha Tsh. 27,034,635,000. Hadi kufikia mwezi Oktoba, 2021 kiasi cha Tsh. 9,271,890,951 Sawa na asilimia 34.30 kilikuwa kimekusanywa.

Aidha kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilikisia kutumia kiasi cha Tsh 27,034,635,000.00 hadi kufikia mwezi Oktoba, 2021 Halmashauri ilitumia kiasi cha Tsh 8,252,778,093 sawa na asilimia 30.53 kilikuwa kimetumika.

Wajumbe walipokea taarifa na kuijadili, walishauri yafuatayo:.

i. Bakaa ya Tshs 22,000,000/= ambayo ipo kwenye akaunti ya mapato ya ndani zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo husika zitumike badala ya kuendelea kukaa kwenye akaunti na kazi zimesima.

ii. Idara ya Mifugo na Uvuvi iainishe maeneo ya maegesho na mialo ili kurahisisha zoezi la kukusanya mapato.

iii. Idara ya mifugo na uvuvi iwasilishe mapendekezo ya kutengeneza beach kwa ajili ya kutengeneza maeneo mazuri ya ukusanyaji wa mapato (ushuru)

iv. Mweka Hazina (W) ashughulikie na kulipa madeni madogomadogo ili kupumguza Idadi ya madeni.

**RASIMU YA MPANGO MKAKATI WA HALMASHAURI KWA MWAKA 2022/2023-2025/2026**

Taarifa ya Rasimu ya Mpango Mkakati wa Halmashauri iliwasilishwa na kupokelewa, Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango alisema, Mpango Mkakati huo utasaidia Halmashauri kubainisha na kutathimini kiwango cha utoaji wa huduma za Halmashauri kwa kubaini mafanikio na vikwazo vinavyoweza kujitokeza katika utendaji kazi wa Halmashauri.

Wajumbe walipokea taarifa na kuijadili, walishauri

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango awape Wakuu wa Idara na Vitengo Rasimu hiyo ili kila idara ipitie na kurekebisha sehemu yake. Baada ya marekebisho iwasilishwe kwa Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango kwa ajili ya kuwasilisha kwenye kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango.

**KUMB.NA. CMT/04/2021/2022/27 MAPOKEZI YA FEDHA ZA UVIKO 19 KIASI CHA TSHS 1,870,000,000.00**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji alisema, Halmashauri imepokea fedha za zitokanazo na UVIKO 19 kiasi cha Tshs. 1,870,000,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Idara ya Elimu Msingi, Elimu Sekondari na Afya. Mchanganuo wa fedha ni kama ifuatavyo:

| NA | IDARA | FEDHA POKELEWA | SHUGHULI ILIYOKUSUDIWA |
|---|---|---|---|
| 1 | UVIKO 19- MSINGI | 140,000,000.00 | Ujenzi wa madarasa ya shule shikizi |
| 2 | UVIKO 19- SEKONDARI | 1,340,000,000.00 | Ujenzi wa madarasa |
| 3 | UVIKO 19- AFYA | 390,000,000.00 | Ujenzi wa Jengo la dharura na nyumba za watumishi |
| | **JUMLA** | **1,870,000,000.00** | |

**KUMB.NA. CMT/04/2021/2022/28 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao, alishauri yale yote yakuyoshauriwa yafanyiwe kazi. Baada ya maelezo hayo alifunga kikao saa 8:00 mchana na kuwatakia wajumbe mapumziko mema.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| MWENYEKITI: | KATIBU: |
| JINA: S. Manyaki | JINA: A. Mshu |
| SAINI: [signature] | SAINI: [signature] |
| TAREHE: 21/12/2021 | TAREHE: 21/12/2021 |